# HOTUBA YA MHE. JAJI (RUFAA) JACOBS C. M. MWAMBEGELE MWENYEKITI WA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI, KWENYE MKUTANO WA TUME NA WADAU WA UCHAGUZI MKOANI MWANZA UNAOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MKUU WA MKOA TAREHE 09 AGOSTI, 2024

- **Mhe. Jaji (Mahakama Kuu) Asina Omari - Mjumbe Wa Tume,**
- **Mhe. Magdalena Rwebangira - Mjumbe Wa Tume,**
- **Mkurugenzi wa Uchaguzi,**
- **Mratibu wa Uandikishaji wa Mkoa,**
- **Wadau wa Uchaguzi,**
- **Watendaji wa Tume,**

- **Waandishi wa Habari,**
- **Mabibi na Mabwana.**

**Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

***Ndugu Wadau!!***

Kwanza kabisa napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukusanyika mahali hapa siku hii ya leo tukiwa wazima wa afya. Kwa niaba ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, ninawakaribisha nyote katika mkutano huu muhimu.

Nawashukuru na kuwapongeza kwa kuwa kualikwa ni jambo moja na kufika ni jambo jingine. Tume inathamini sana uwepo wenu kwa kuwa ni sehemu ya mafanikio ya kile tulichokusudia kuzungumza siku ya leo.

Pili na kwa umuhimu nawashukuru, kwa jinsi ambavyo mmekuwa mkitupa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu ya Tume haswa katika michakato ya uchaguzi. Tume inatarajia kupata ushirikiano mkubwa zaidi kutoka kwenu, kwa kuwafikishia wananchi wa mkoa wa Mwanza taarifa sahihi na kwa wakati zinazohusu zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na kuwahamasisha wananchi wenye sifa ya kujiandikisha kuwa wapiga kura, wajitokeze kwa wingi kwa tarehe ambazo Tume imeziweka kwa kila kituo.

***Ndugu Wadau!!***

Nawapongeza sana ninyi wadau wa uchaguzi na wananchi wa Mkoa wa Mwanza kwa kupata fursa ya mkoa wenu kuwa katika mzunguko wa tatu wa uboreshaji wa Daftari. Kama mnavyofahamu kufanikiwa kwa zoezi lolote kunatokana na ushiriki wa wadau. Hivyo, ni matarajio ya Tume kuwa mtakuwa mabalozi wazuri wa kusambaza taarifa na kuhamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kujiandikisha na kuboresha taarifa zao ili zoezi hili lifanyike kwa ufanisi na kwa mafanikio makubwa.

***Ndugu Wadau!!***

Lengo la kukutana kwetu leo ni kupeana taarifa mbalimbali za maandalizi kwa ajili ya kuanza kwa zoezi la uboreshaji

wa Daftari. Maandalizi hayo pamoja na mambo mengine yanajumuisha uhakiki wa vituo vya kuandikisha wapiga kura, uboreshaji wa majaribio, ununuzi wa vifaa na ushirikishwaji wa wadau kama tunavyofanya hapa leo.

Katika mkutano huu Mkurugenzi wa Uchaguzi pia atakuwa na mada itakayo zungumzia uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Wataalamu wa TEHAMA watawapitisha kwenye mfumo wa uandikishaji na vifaa vitakavyotumika.

***Ndugu Wadau!!***

Sote tunafahamu kuwa nchi yetu ipo katika maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. Katika maandalizi hayo, Tume chini ya ibara ya 74(6) ya Katiba ya Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, imepewa mamlaka ya kutekeleza majukumu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na jukumu la Kusimamia na Kuratibu Uandikishaji wa Wapiga Kura kwa ajili ya Uchaguzi wa Rais na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano na Madiwani kwa Tanzania Bara.

Jukumu hilo pia, limeainishwa kwenye kifungu cha 16(5) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024 ambacho kinaweka sharti kwa Tume kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mara mbili kati ya uchaguzi mkuu uliomalizika na kabla ya siku ya uteuzi wa wagombea kwa ajili ya uchaguzi mkuu unaofuata.

***Ndugu Wadau!!***

Kama mnavyofahamu, Tume tayari imeanza zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ambapo uzinduzi ulifanyika mkoani Kigoma tarehe 20 Julai, 2024 na mgeni rasmi alikuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (MB). Uzinduzi huo uliend sambamba na kuanza kwa mzunguko wa kwanza wa uboreshaji kwenye mikoa mitatu ya Kigoma, Tabora na Katavi na kufuatiwa na mzunguko wa pili ambao umejumuisha mikoa ya Geita na Kagera. Uboreshaji wa Daftari kwa sasa unaendelea kwenye mikoa hiyo ya Kagera na Geita hadi tarehe 11 Agosti, 2024.

Aidha, mzunguko wa tatu wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura utajumuisha mkoa huu wa Mwanza na Shinyanga ambapo uboreshaji utaanza tarehe 21 hadi 27 Agosti, 2024. Vituo vitafunguliwa kuanzia saa 2:00 asubuhi na kufungwa saa 12:00 jioni.

***Ndugu Wadau!!***

Kama mnavyokumbuka kati ya tarehe 24 hadi 30 Novemba, 2023, Tume ilifanya uboreshaji wa majaribio katika Kata ya Ikoma iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Rorya, Mkoa wa Mara na Kata ya Ng'ambo iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, mkoani Tabora. Lengo la majaribio hayo yalikuwa ni kupima uwezo wa vifaa na mi-

fumo ya uandikishaji itakayotumika wakati huu wa uboreshaji wa Daftari.

Uboreshaji huu wa majaribio ulifanyika kwa mafanikio kutokana na kuboreshwa kwa vifaa na mifumo ya uandikishaji wa wapiga kura.

Pamoja na mafanikio hayo, kulikuwa na changamoto ndogo ya baadhi ya wapiga kura waliokuwa wanaboresha taarifa zao kusahau majina yao waliyojiandikisha awali walipokwenda vituoni kurekebisha taarifa zao na hivyo kuchukua muda mrefu kituoni kutokana na ugumu wa kupata taarifa zao kwa haraka.

***Ndugu Wadau!!***

Uboreshaji huu kama ilivyokuwa uboreshaji wa mwaka 2015 na 2020, utahusisha matumizi ya teknolojia ya Biometric Voters' Registration (BVR). Mfumo wa teknolojia hii ya BVR hutumika katika kumtambua mtu na kumtofautisha na mwingine. Uandikishaji huu wa wapiga kura utahusisha uchukuaji wa alama za vidole vya mikono, picha na saini na kuhifadhiwa kwenye kanzidata ya wapiga kura.

Hata hivyo, tofauti na mwaka 2015 na 2020, uboreshaji wa Daftari wa mwaka 2024/25 utatumia teknolojia ya *BVR Kits* zilizoboreshwa kwa kuwekewa program endeshi ya kisasa zaidi. Vilevile, *BVR Kits* zitakazotumika zimepunguzwa uzito ambapo zitakuwa rahisi kubebeka na kufanya zoezi

la uboreshaji wa Daftari kuwa rahisi haswa kwenye maeneo ya vijijini ambapo watendaji hulazimika kubeba vifaa kwa umbali mrefu. **Mkurugenzi wa Uchaguzi atatoa maelezo ya kina kuhusu maboresho haya wakati wa kuwasilisha mada.**

***Ndugu Wadau!!***

Tume katika kuhakikisha kwamba inaenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia ikiwa ni pamoja na kurahisisha zoezi hili la uboreshaji wa Daftari, imeboresha mfumo wa uandikishaji ambao kwa mara ya kwanza utamwezesha mpiga kura aliyepo kwenye Daftari kuanzisha mchakato wa kuboresha taarifa zake au kuhama kituo kwa kutumia aina zote za simu au kompyuta.

Aidha, kwa wanaotumia simu za kawaida (maarufu kama kitochi au kiswaswadu) nao wanaweza kutumia huduma hii kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha watabonyeza namba **9** halafu wataendelea na hatua zingine kama itakavyokuwa inaelekezwa kwenye simu husika.

Mtumiaji wa huduma hii, atatakiwa kufika kituo anachokusudia kujiandikisha ili akamilishe hatua za kupigwa picha, kuweka saini na kupatiwa kadi yake ya mpiga kura.

***Ndugu Wadau!!***

Kwa mujibu wa kifungu cha 9(1) na (2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024, uboreshaji wa Daftari utahusu kuwaandikisha raia

wa Tanzania waliotimiza umri wa miaka kumi na nane na zaidi au watakaotimiza umri huo wakati au kabla ya tarehe ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 na ambao hawajapoteza sifa kwa mujibu wa sheria ya uchaguzi au sheria nyingine yeyote.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 168 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024 **kadi za mpiga kura zilizotolewa mwaka 2015 na 2020 zenye jina la Tume ya Taifa ya Uchaguzi ni halali na zitaendelea kutumika kwenye chaguzi zijazo. Hivyo, zoezi hili la uboreshaji wa Daftari haliwahusu wapiga kura wenye kadi hizo.**

***Ndugu Wadau!!***

Ningependa kusisitiza kuhusu suala la kujiandikisha kuwa mpiga kura zaidi ya mara moja, jambo hili ni kosa la kisheria kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 114(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024, kifungu hicho kinasema kuwa, mtu yeyote atakayeomba kuandikishwa zaidi ya mara moja atakuwa ametenda kosa la kisheria na akitiwa hatiani adhabu yake ni faini isiyopungua kiasi cha shilingi laki moja (100,000/=) na isiyozidi shilingi laki tatu (300,000/=) au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Hivyo, nitoe rai kwenu, muwaelimishe wananchi wanaokwenda vituoni kwa ajili ya kuomba kuandikishwa

kuwa wapiga kura, kuomba kuandikishwa kuwa wapiga kura mara moja tu ili kuepuka uvunjaji wa sheria.

***Ndugu Wadau!!***

Tume imeweka utaratibu kwa watu wenye ulemavu, wazee, wagonjwa, wajawazito na wakina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao vituoni kupewa fursa ya kuhudumiwa bila kupanga foleni. Hivyo, Tume inawaomba wadau wa uchaguzi muwafahamishe wananchi wote waliopo kwenye makundi tajwa kujitokeza kwa wingi kwenda kujiandikisha au kuboresha taarifa zao vituoni kwa kuwa utaratibu mzuri wa kuwahudumia umewekwa.

***Ndugu Wadau!!***

Tume chini ya kifungu cha 10(1)(g) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya Mwaka 2024, imepewa jukumu la kutoa elimu ya mpiga kura nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, imejipanga kuhakikisha kuwa wananchi wanapata uelewa wa kutosha kuhusu uboreshaji huu.

Njia mbalimbali za kutoa elimu ya mpiga kura zitatumika ili kuhakikisha kwamba wadau wote wanapata fursa ya kuelimika na kuelewa mambo yote ya msingi kuhusu uboreshaji huu ili wajitokeze kwa wingi kushiriki kwenye zoezi hilo.

***Ndugu Wadau!!***

Tume imekuwa na utaratibu wa mara kwa mara wa kuwashirikisha wadau wa uchaguzi wakati wa utekelezaji wa majukumu yake. Leo tumekutana na ninyi wadau wa uchaguzi wa Mkoa wa Mwanza, kati ya tarehe 07 hadi 15 Juni, 2024 tulikutana na wadau wa uchaguzi ngazi ya Taifa mkoani Dar es Salaam. Mikutano kama hiyo imeshafanyika mkoani Kigoma, Katavi, Tabora, Geita na Kagera na itaendelea kufanyika kwenye mikoa yote kulingana na ratiba ya uboreshaji.

Wadau hao ni pamoja na Viongozi wa vyama vya siasa, Viongozi wa Dini, Wawakilishi wa Asasi za Kiraia, Wahariri wa vyombo vya habari, Waandishi wa habari, Maafisa Habari wa Mikoa na Halmashauri, Wawakilishi

wa Makundi mbalimbali ya Vijana, Watu wenye ulemavu, Wanawake na Wazee wa Kimila.

Lengo la mikutano hii ni kuwapa taarifa za uwepo wa zoezi hili na kuwapitisha katika vifaa na mifumo ya uandikishaji pamoja na kuona namna zoezi litakavyofanyika vituoni.

Aidha, kila chama cha siasa kimepewa nakala ya orodha ya vituo vyote vya kuandikisha wapiga kura. Dhumuni la kuwapatia nakala hizo ni kuwawezesha kupanga na kuweka mawakala wa uandikishaji katika vituo vya kuandikisha wapiga kura.

Kila chama kitaruhusiwa kuweka wakala mmoja kwenye kituo cha kuandikisha wapiga kura kwa lengo la kushuhudia utekelezaji wa zoezi la uboreshaji kituoni

ikiwemo kuwatambua wale wanaokuja kituoni kama wana sifa za kuandikishwa.

Niwaombe wadau wa uchaguzi kwa umoja wenu kuzingatia sheria za uchaguzi, kanuni za uboreshaji na maelekezo ya Tume kuhusu zoezi la uboreshaji wa Daftari. Tume kwa upande wetu tutazingatia Katiba, sheria ya uchaguzi na kanuni zilizotungwa chini ya sheria katika zoezi hili la uboreshaji.

***Ndugu Wadau!!***

Kwa kumalizia, ninapenda tena kuwashukuru wote kwa kuhudhuria mkutano huu. Ni vyema mkatambua kuwa uboreshaji huu unamhusu kila mwananchi mwenye sifa ya kuandikishwa kuwa mpiga kura na anayeboresha taarifa

zake. Hivyo, natoa rai kwenu kuwahimiza wananchi kupitia majukwaa yenu ya kisiasa, kijamii, kitamaduni, kiimani na kiuchumi wajitokeze kwa wingi kujiandikisha na kuboresha taarifa zao kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Ni mategemeo yetu kuwa michango na maoni mtakayotoa leo yatakuwa na manufaa makubwa katika kutekeleza zoezi ambalo lipo mbele yetu.

***Ndugu Wadau!!***

Kauli mbiu yetu ya uboreshaji wa Daftari la kudumu la Wapiga Kura kwa mwaka 2024/25 inasema **"KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA"**

**Baada ya kusema hayo, sasa napenda kutamka rasmi kuwa mkutano wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi na Wadau wa Uchaguzi Mkoa wa Mwanza umefunguliwa!!**

*AHSANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA!!*